Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 3, Issue 2
29th Shawwal 1431
8th October, 2010

Yaliyomo

Kulingania Katika Njia Ya Allaah 1– 3

Damu Asilia za wanawake 4

KULINGANIA KATIKA NJIA YA ALLAAH (عزّ وجلّ)

Mtayarishi: Sheikh Saalih al-Fawzaan

Ulinganizi wa Allaah (عزّ وجلّ) umetulia juu ya nguzo thabiti na zimethubutu juu ya misingi iliyo muhimu bila ya shaka yoyote. Iwapo patakosekana chochote katika misingi hiyo, da'wah haitokuwa ni ya kisawasawa, wala haitoleta natija ipendekezayo—hata kama kumetumika juhudi kubwa aina gani, wala muda gani umepotezwa. Huu ni ukweli ambao tunaoushuhudia kuhusiana na ulinganizi mwingi unaotekelezwa siku hizi, ambao hauungwi mkono na nguzo hizo, wala usiokuwa umejengwa juu ya misingi hiyo. Misingi hii yenye kuunga mkono da'wah ya kisawasawa inaoyeshwa waziwazi kwenye Kitaab na Sunnah, na inaweza kufupishwa kwa mukhtasar kama ifuatavyo:

Ujuzi Wa Lile Analolilingania Mtu

Kwa vile mtu mjinga hafai kuwa ni da'ee (mlinganizi), Allaah (عزّ وجلّ) alimwambia Mtume wake (صلى الله عليه وسلم): **"Sema: Hii ni njia yangu nawaita watu kwa Allaah (kumuabudu yeye peke yake) kwa ujuzi (*Baseerah*) mimi na anayenifuata."** [Yusuf 12:108].

Na *Baseerah* ni 'ilmu. Kwahivyo *daa'ee* anakuwa na yakini anapopambana na wale ambao ni wanavyuoni wa upotofu, ambao watakaomletea ushawishi na ugomvi usoleta manufaa, kwa min-ajil ya kuukanusha ukweli, na Allaah (عزّ وجلّ) amesema: **"Na bishana nao (wanaokukhalifu) kwa yaliyo bora."** [an-Nahl 16:125].

La ziyada ni kwamba, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwambia Mu'aadh: "*Wewe unakwenda kwa watu walio miongoni mwa Watu Wa Kitaab.*"

Kwahivyo, iwapo *daa'ee* hatojiandaa na 'ilmu yenye kumtosheleza yeye katika kupambana na shaka, na kubishana na mpinzani, basi atashindwa kwenye mapambano ya mwanzo na atazuiwa mwanzoni mwa njia.

Kutenda Kulingana Na Lile Analolilingania

Ili yeye awe ni mfano bora—vitendo vyake vithibitishe maneno yake, na asiwape sababu wapinzani wa haki. Allaah (عزّ وجلّ) alisema kumuhusu Mtume wake Shu'ayb (عليه السلام) yakwamba aliwaambia watu wake: **"Na wala sitaki kuwakhalifu nyinyi kwa ambayo ninawakataza, sikuwa mimi ila nataka wema kadiri ya uwezo wangu."** [Hud 11:88]

Na Allaah (عزّ وجلّ) alimwambia Mtume wake Muhammad (صلى الله عليه وسلم): **"Sema, hapana shaka Swala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu (zote) ni kwa Allaah ambaye ni Muumba wa walimwengu. Hana mshirika na kwa hilo nimeamrishwa na mimi ni wa mwanzo wa wenye kusilimu (katika Umma huu).** [al-An'aam 6:162-163]

"Ni nani aliye mzuri wa maneno kuliko anayewaita watu katika kumuabudu Allaah peke yake na akafanya mema." [Fussilat 41:33]

Al-Ikhlaas (Utakaso Wa Niya)

Kiasi cha kwamba *Da'wah* ifanywapo kwa utakaso na kwa ikhlasi kwa ajili ya Uso wa Allaah (عزّ وجلّ) na kutarajia malipo mema. Haifanywi kwa kujionyesha, wala kusifiwa, wala kutaka jaha, wala kutaka uongozi, wala kutaka malengo ya kilimwengu—kwani iwapo yoyote katika malengo haya yatakapo changanyika na Da'wah, basi Da'wah hiyo haitokuwa ni kwa utakaso wa Allaah (عزّ وجلّ); bali utakuwa ni ulinganizi wa mtu binafsi, au kwa kujipatia malengo ya kilimwengu, kama alivyotupasha habari Allaah (عزّ وجلّ) yakwamba Mtume wake alisema: **"Sitaki kwenu malipo kwa ninayowafikishia hii Qur'aan."** [al-An'aam 6:90]

"Sitaki mali (kwa hii kazi yangu)" [Hud 11:29]

Kuanzia Na Lenye Umuhimu Wa Kimsingi, Kisha Ni Kwa Litakalo Fuata Baada Ya Hilo Kwa Umuhimu, Na Namna Hiyo.

Kwahivyo, kwanza analingania kwenye kurekebisha *'aqeedah* (Manhaj Na Imaan), kwa kuamrisha yakwamba ibada zote hufanywa kwa kumtakasia Allaah (عزّ وجلّ), na kwamba Shirk

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

KULINGANIA KATIKA NJIA YA ALLAAH (عزّ وجلّ)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

imeharamishwa. Kisha kuamrisha kusimamisha Swala, na kulipa Zakaah, na kwamba uwajibikaji uliofaradhishwa unatekelezwa na kwamba mambo yaliyoharamishwa huepukwa. Huu ndiwo mfumo uliofuatwa na Mitume wote, kama alivyosema Allaah: **"Na Wallaahi hakika tulipeleka katika kila Umma Mtume kwamba hapana shaka muabuduni Allaah. Na jiepusheni kuabudu asiyekuwa Allaah."** [an-Nahl 16:36]

"Hatukumpeleka kabla yako wewe (Muhammad) Mtume yeyote ila tulimpelekea wahyi, (ufunuo) kwamba hapana shaka ya jambo hapana apasaye kuabudiwa kwa haki ila mimi basi nipwekesheni katika ibada." [al-Anbiyaa 21:25]

Zaidi ya hayo, Mtume alipompeleka Mu'aadh Yemen, alisema kumwambia: *"Kwa hakika unakwenda kwa watu miongoni mwa Watu Wa Kitaab, kwahiyo anza kuwalingania wakiri yakwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah na Muhammad ni Mtume wake. Kwahiyo, watakapokubali hayo, kisha wapashe habari yakwamba Allaah amefaradhisha swala tano juu yao katika kila mchana na usiku wake."*

Kisha kunapatikana kwenye njia yake na utaratibu wa ulinganizi wa katika *Da'wah*, mfano ulio bora na mfumo uliokamilika kisawasawa – kwa sababu alibakia Mjini Makkah kwa miaka kumi na tatu, akiwalingania watu kwenye *tawheed* na kuwakataza na mambo ya *Shirk* (Ushirikina), kabla ya kuwaamrisha kuswali, kutoa zakaah, kufunga na kwenda kuhiji Makkah, na kabla ya kuwakataza mambo ya riba, uzinifu, wizi na mauaji.

Kuvumilia Kwa Kusubiri Unapopambana Na Matatizo Yenye Kutokea Katika Ulinganizi Wa Allaah, Na Unapopambana Na Madhara Kutoka Kwa Watu

Kwani njia ya da'wah haikupambwa na mauwa ya mawaridi, bali imefunikwa na taabu na mambo ya hatari. Mfano bora wa haya ni hali ya Mitume (صلوات الله وسلامه عليهم) – kuhusiana na madhara na istihzai kutoka kwa watu wao. Kama Allaah (عزّ وجلّ) alivyomwambia Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم): **"Na Wallaahi hakika walifanyiwa istihzai Mitume wengi kabla yako wewe. Na, ilithubutu kuadhibiwa ambao waliofanya istihzai kwa sababu ya istihzai zao."** [al-An'aam 6:10]. Na akasema: **"Na Wallaahi hakika walikanushwa Mitume wengi kabla yako wewe na walisubiri kwa waliokanushwa kwayo na waliudhiwa mpaka ilipowajia wao nusra yetu."** [al-An'aam 6:34].

Vilevile wafuasi wa Mitume walikumbana na madhara kama hayo na tabu, kwa kuwiana na juhudi zao za kulingania kwa Allaah (عزّ وجلّ) wakiandama mifano ya Mitume Watukufu (صلوات الله وسلامه عليهم)

Mlinganizi Inamlazimu Awe Ni Mtu Mwenye Tabia Njema, Mwenye Kutumia Hikma Katika Ulinganizi Wake.

Kwa vile jambo hili ndilo litakalokuwa ni sababu muhimu ya kukubaliwa ulinganizi wake. Kama ambavyo Allaah (سبحانه وتعالى) alivyowaamrisha Mitume wake wawili, Musa na Haarun (عليهما السلام) yakwamba huu ndiwo mfumo watakaoutumia kupambana na Makafiri waliokuwa waovu mno juu ya Uso wa ardhi hii. Fir'aun aliyejidai Uungu yeye Mwenyewe. Allaah (عزّ وجلّ) akasema: **"Na muambieni maneno ya Upole huwenda akawaidhika au akaogopa."** [Twaa-haa 20:44].

Na Allaah (عزّ وجلّ) akamwambia Musa (عليه السلام): **"(Alimwambia): Nenda kwa Fir'aun hapana shaka yeye amekiuka mipaka kwa jeuri zake. Na uwaambie, jee waonaje ujitakase nafsi yako (na madhambi). Na nikuonyeshe njia ya kuelekea kwa Mola wako ikawa ni sababu ya kumcha yeye."** [an-Naazi'aat 79: 17-19].

Na akasema Allaah (عزّ وجلّ) kumuhusu Mtume wake Muhammad (صلى الله عليه وسلم): **"Ni kwa sababu ya rehma itokayo kwa Allaah ulikuwa laini kwao. Na lau ungekuwa ni mkali, mgumu wa moyo basi wangelikukimbia walio pembeni (karibu) nawe."** ['Aali-Imraan 3:159].

"Na hapana shaka yako, una tabia nzuri." [al-Qalam 68:4]

"Waite (watu wote) katika dini ya Mola wako kwa usemi wa busara na mawaidha mazuri. Na bishana nao (wanaokukhalifu) kwa yalio bora." [an-Nahl 16:125]

Mlinganizi Ni Lazima Asimame Imara Kwenye Matarajio Yake Na Atumainie Mambo Mazuri

Haitakikani akate tamaa ya ta'athira ya ulinganizi wake, wala ya uongofu wa watu wake. Wala asikate tamaa ya usaidizi wa Allaah (عزّ وجلّ) hata baada ya kupita muda mrefu. Na tena, anacho kielelezo bora cha Mtume wa Allaah katika mas'ala haya. Kwahiyo Mtume wa Allaah (عزّ وجلّ) Nooh (عليه السلام) alibaki miongoni mwa watu wake kwa muda wa miaka mia tisa na khamsini, akiwalingania kwa Allaah (عزّ وجلّ)

Vilevile, yalipokuwa madhara na unyanyasaji ulosababishwa na makafiri yamezidi, na Mjumbe wa Milima alipokuja kwa Mtume wetu Muhammad (صلى الله عليه وسلم) kumuuliza iwapo alimtaka awafinyange kwa Milima ile miwili alimjibu: *"Laa! Mimi naonelea niwe na subira nao. Huwenda*

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

KULINGANIA KATIKA NJIA YA ALLAAH (عزّ وجلّ)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

Allaah akaleta kizazi kutokamana na wao, ambacho kitakachomuabudu Allaah Peke Yake, pasi na kumfanyia mshirika yoyote."

Kwahiyo, iwapo *da'ee* atakosa sifa hii, basi atakwama mwanzoni mwa njia na avunjike moyo na kutafshika. Kwahivyo, ulinganizi wowote ulokosa kujengwa juu ya misingi hii, na ambao *manhaj* (mfumo) yake sio mfumo wa Mitume basi utakuwa ni wenye kuvunja moyo na hautofaulu, na itakuwa ni kazi ya sulubu isiyokuwa na faida yoyote. Dalili ya wazi kabisa ya mambo haya ni zile *jamaa'ah* (makundi) za kileo yenye kujitengezea mifumo na mipangilioyao wenyewe na *da'wah* zao, ambazo ni tafauti na mifumo ya Mitume. Makundi haya yamepuuza umuhimu wa 'aqeedah (Imani za sawa na *manhaj*) – isipokuwa wachache miongoni mwao – na badala yake wakilingania kwenye kurekebisha mas'ala madogo yasiyokuwa na umuhimu. Kwahiyo kundi moja hulingania kwenye kurekebisha mas'ala ya utawala na siyasa na kupigania kuanzishwa *hudood* (adhabu za kisheriya), na kwamba *Sharee'ah* (Hukmu za ki-Islamu) zinapasa kutekelezwa katika kuwahukumu watu – na kwa hakika mambo haya ni muhimu sana, lakini si muhimu zaidi: Kwani atawezaje mtu kutafuta na kuthibitisha kuzitekeleza hukmu za Allaah juu ya mwivi na mzinifu, kabla ya kutafuta kuzithibitisha na kuzitekeleza hukmu za Allaah juu ya *mushrik* – mwenye kumshirikisha Allaah (عزّ وجلّ). katika ibada na wengine. Twawezaje sisi kudai yakwamba hukmu ya Allaah itekelezwe juu ya watu wawili wenye kugombania Kondoo au Ngamia, kabla ya kudai yakwamba hukmu ya Allaah itekelezwe juu ya wale wenye kuabudu masanamu na makaburi na wale wenye kukanusha au kushikilia imani za uzushi kuhusiana na Majina ya Allaah na Sifa zake – kuzinyan'ganya na kuzivua maana zake za kweli, au kuzipotosha. Jee! watu hawa si waovu wakubwa kuliko wale wenye kuzini, kunywa mvinyo na kuiba?!! Kwani hizo ni hatia dhidi ya mwana-adamu, haliyakuwa *shirk* na ukanushaji wa Majina ya Allaah na Sifa zake ni hatia dhidi ya Muumba – Aliye epukana na kila aina ya upungufu na haki ya Muumba ina kipa-umbele juu ya haki za viumbe. Sheikh ul Islaam, Ibn Taymiyyah (k. 728H), amesema kwenye kitabu chake: *al-Istiqaamah* (1/466): "Kwahiyo, madhambi haya yakiandamana na *tawheed* iliyo ya sawa ni bora kuliko *tawheeh* yenye ufisadi inayoandamana na kukosekana kwa madhambi hayo."

Kisha *jamaa'ah* (kundi) nyengine inayojinasibisha na *da'wah*, isipokuwa yakwamba mfumo wao vilevile unapingana na mifumo ya Mitume. Hawaupi umuhimu wowote '*aqeedah* iliyo ya sawa, bali huyapa umuhimu baadhi ya vitendo fulani vya '*Ibada* na kutekeleza dhikr (kumkumbuka Allaah (عزّ وجلّ) kwenye njia za ki-Sufi. Wanajishughulisha na khurooj (kutoka nje) na kuzuru miji tafauti. Yaliyo muhimu kwao ni kwamba wameweza kuwavutia watu wajiunge nao bila ya kujali kuhusu '*aqeedah* zao. Na njia zote hizi ni za uzushi, wakichukulia kama alama zao za kuanzia, mas'ala ambayo yaliyowachwa mpaka dakika za mwisho katika ulinganizi wa Mitume. Hii ni kama katika hali ya mtu mwenye kutafuta njia za matibabu ya mwili ambao kichwa chake kimekatwa – kwani mahali pa '*aqeedah* katika dini, ni kama kichwa kuhusiana na mwili.

Kwahiyo ni muhimu kwa makundi haya warekebishe fikra zao na ufahamu, kwa kurejea nyuma kwenye Kitaab na Sunnah, kwa min-ajil ya kuujua mfumo ya Mitume katika ulinganizi wa Allaah (عزّ وجلّ) Kwani kwa hakika, Allaah – aliye epukana na kila upungufu – ametupasha habari yakwamba mamlaka kamili na kujitawala, ambao ndio sehemu ya kati na kati za ulinganizi wa jamaa'ah iliyotangulia ambayo tuliyoitaja, haiwezekani kupatikana isipokuwa baada ya '*aqeedah* ya sawa, kiasi cha kwamba ibada zote zimstahiki Allaah (عزّ وجلّ) Peke yake na kuabudu chochote chengine kimekatazwa. Amesema Allaah (عزّ وجلّ: **"Amewaahidi Allaah walioamini katika nyinyi na kufanya mambo mema, Wallaahi atawafanya, atawafanya ni makhalifa (watawala) kama alivyo-wafanya makhalifa waliowatangulia nyinyi. Na Wallaahi atawamakinishia, atawamakinishia dini yao kwa aliyowaridhia nayo na Wallaahi atawabadilishia, atawabadilishia ya hofu yao; amani waniabudu mimi, na wasinishirikishe na kitu chochote, na atakayekanusha baada ya hizi neema hao ndio wenye kutoka katika twaa ya Allaah."**

Kwahiyo, watu hawa wanatamani kusimamisha Serikali ya ki-Islamu kabla ya kuzitakasa ardhi zenye imani za *ushirikina* zenye kujichukulia mifumo ya kuwaabudu waliokufa, na kuyaomba makaburi – kama ilivyokuwa haina tafauti na ibada za *al-Laat*, *al-'Uzza* na wa tatu wao *Manaat*, bali hii yao ni mbaya zaidi. Kwahivyo, wanajaribu jambo ambalo lisilowezekana:

"Na yeyote mwenye kutafuta utukufu bila ya kufanya juhudi na bidii, atakuwa akijipotezea maisha yake katika kutafuta jambo lisilowezekana."

Kwa hakika, usimamishaji na utekelezaji wa *Sharee'ah* na hukmu za adhabu, na kusimamisha Serikali ya ki-Islamu, na kujiepusha na kila kilichoharamishwa, na utekelezaji wa kila kilichowajibishwa – mambo yote haya ni katika haki za *tawheed*; na mas'ala yenye kuikamilisha na kuifuatilizia kutokana nayo. Sasa twawezaje kujishughulisha na lile ambalo ni (kitu) tanzu, haliyakuwa tulipuuze lile ambalo ni lenye umuhimu wa kimsingi?

Umm Salamah (رضي الله عنهما) alimuuliza Mtume (صلى الله عليه وسلم) "Mimi ni mwanamke mwenye nywele zilizosukwa kwa mkazo juu ya kichwa changu; jee, nizifungue nikitaka kuoga, kutokana na kujamiiana (*au kwa ajili ya heidh kama ilivyo kwenye riwaya moja*)?". Mtume (صلى الله عليه وسلم)akasema: "Laa, itatosha kwako kunyunyiza (kueneza) maji mara 3 juu ya kichwa chako, kisha uwende kujimwagia maji kwa wingi juu ya kiwiliwili chako chote ambapo utakuwa umetwahirika kama ipasavyo."

Mas'ala: Ikiwa mwanamke mwenye heidh atatwahirika akiwa ndani ya muda wa kisheriya unaompasa kutekeleza swala, basi atawajibika kuoga haraka iwezekanavyo ili aweze kutekeleza swala yake katika wakati unaofaa. Ikiwa alikuwa kwenye safari na hapakuwa na uwezekano wa kupata maji au huwenda akadhurika (kwa ajili ya sababu fulani: maradhi au vyenginevyo) kwa kuyatumia maji yaliyoko, basi anaweza kutekeleza Tayammum mpaka zile sababu zinazomzuiya kutumia maji ziondolewe. Hapo itambidi kuoga.

Mas'ala: Kuna baadhi ya wanawake ambao hutwahirika wakati wa kuwajibika kuswali lakini wao huakhirisha kuoga wakidai yakwamba hawawezi kumaliza kujisafisha wakiwa ndani ya wakati inapowapasa kuswali! Hii ni sababu tu wanayotafuta, kwa sababu anaweza kutekeleza vitendo vya kuwajibika katika Ghusl vinavyomfanya awe ametwahirika na akaweza kutekeleza swala yake kwa wakati wake. Kisha anaweza kutekeleza Ghusl kwa ukamilifu atakapokuwa na wasaa.

Istihaadhah Na Hukmu Zake

ISTIHAADHAH ni kutoka kwa damu katika tupu ya mwanamke kiasi cha kwamba isisimame au inaweza kusimama lakini kwa muda mchache (siku au siku mbili katika kila mwezi).

Damu Isiyosimama: 'Aaisha (رضي الله عنهما) amesimulia yakwamba Faatimah Bint Abee Hubaish alimwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Ewe mjumbe wa Allaah! Mimi sitwahiriki (yaani; damu yanitoka mfululizo) na katika riwaya moja "napata heidh (baina ya ada zangu) wala sitwahiriki."

Damu Inayosimama Kwa Wakati Wa Muda Mchache

Humnah Bint Jahsh alimjia Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: "Mimi hupata damu ya Istihaadhah kwa wingi tena hutoka kwa nguvu."

Hali za mwenye Istihaadhah

Kuna hali aina tatu za mwenye Istihaadhah:

Hali Ya Kwanza: Ikiwa mwanamke ana ada yake ya kila mwezi ya heidh yenye kujulikana kabla ya kuingia kwenye Istihaadhah. Mwanamke kama huyo na arudie katika muda wa heidh yake iliyopita yenye kujulikana na ashikamane na muda huu. Hatimae hukmu za heidh zitawajibika kwake. Ama kuhusu masiku ya ziyada yatazingatiwa kuwa Istihaadhah ambayo yatachukuwa hukmu za Istihaadhah ifikapo zamu yake. Mfano wa hali kama hiyo ni: Mwanamke aliyekuwa na mazoeya ya kupata ada yake kwa siku sita kuanzia kila mwanzo wa mwezi. Hatahivyo, mara ikatokea yakwamba damu ya Istihaadhah ikamsibu na akaanza kuipata kwa mfululizo. Hukmu ni kwamba mwanamke kama huyo ataanza kuhesabu ada yake ya mwezi kuwa ni siku sita tu kuanzia mwanzo wa mwezi. Masiku ya ziyada yatazingatiwa kuwa Istihaadhah ambayo ifikapo zamu yake yatachukuwa hukmu za Istihaadhah.

Ukweli umedhihirishwa kwenda sambamba na aathaar ya 'Aaisha (رضي الله عنهما) yakwamba Faatimah Bint Abu Hubaish (رضي الله عنهما) alisema: "Ewe Mjumbe wa Allaah! Mimi natokwa na damu ya Istihaadhah kwa nguvu na matokeo yake ni kwamba sitwahiriki. Jee, niwache kuswali?" Mtume (صلى الله عليه وسلم): Akamjibu: "Laa, kwa sababu hiyo ni damu itokayo kwenye mshipa ('Irq), lakini usiswali kwa muda wa masiku yatakayokuwa sawa na yale ambayo ulikuwa ukipata ada yako ya kila mwezi, kisha tekeleza Ghusl (kaoge) na uswali."

Kuna riwaya nyengine katika Saheeh Muslim yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwambia Umm Habeebah Bint Jahsh (رضي الله عنهما) aliyekuwa akitokwa na damu ya kuendelea: "Kaa kwa muda ulio sawa na ada yako ya mwezi; kisha baadae jitwahirishe, na uswali." Wala usijali kuhusu damu ya ziyada.

Hali Ya Pili: Mwanamke anapokosa ada ya kila mwezi ya heidh kabla hajaingia kwenye Istihaadhah kwa maana yakwamba damu ya Istihaadhah imekuwa ikiendelea kumtoka mfululizo tangu mara ya kwanza alipoiona damu hiyo ikimtoka. Mwanamke huyu mwenye hali kama hii atakuwa kwenye nafasi ya kutumia njia ya kupambanua (kutafautisha), yaani; muda wa ada yake ya mwezi utatambulika kwa damu kuwa ya rangi nyeusi au nzito au ya harufu fulani ambayo zote hizo zitakuwa na hukmu moja yenye kutumika kwa damu ya heidh. Damu itakayothubutu kutambulika kuwa kinyume chake itabainika kuwa ni damu ya Istihaadhah iliyo na hukmu zake.

[Endelea Katika Makala Yajayo].

P. O. Box 85477,
Mombasa,
Kenya.

E-mail: info@qssea.net

QSS (E.A)

جمعية القرآن والسنة في شرق إفريقيا

Tuko katika Tovuti
http://www.qssea.net